TANGAZO LA SERIKALI NA. 751 la tarehe 23/8/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (USAFI WA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YA MWAKA 2024

Jina

TS Na 363 la /2017

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2024 na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka, 2017 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 4 kwa kuongeza kanuni ndogo zifuatazo mara baada ya kanuni ndogo ya (3):

"(4) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukasimisha jukumu la usimamizi na usafi wa mazingira kwa viongozi wa mitaa ndani ya Halmashauri.

(5) Mitaa itaweka utaratibu unaofaa wa kukusanya taka ngumu na kuzipeleka dampo na kukusanya ushuru wa uzoaji taka.".

Marekebisho ya kanuni ya 5

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa kuongeza kanuni ndogo zifuatazo mara baada ya kanuni ndogo ya (4):

"(5) Mtu, kampuni au taasisi yoyote inayohitaji kuteketeza vifaa chakavu au bidhaa iliyokwisha muda wa matumizi atalipa gharama ya shilingi laki tatu kwa ajili ya kutumia eneo la Halmashauri la kuteketezea

taka.

(6) Mtu, kampuni au taasisi yoyote inayohitaji kumwaga maji taka katika eneo maalumu lilotengwa na Halmashauri atalipa gharama ya shilingi elfu thelathini kwa tripu moja.”.

Marekebisho ya Jedwali

4. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza kama ifuatavyo:

(a) kwa kufuta maneno “ada ya huduma ya dampo ya Shilingi 15.000/=” katika aya ya 4 na badala yake kuweka maneno “ada ya dampo Shilingi 10,000/=”;

(b) kwa kufuta maneno “nyumba ya kuishi” katika aya ya 7 na badala yake kuweka neno “kaya”;

(c) kwa kuongeza aya zifuatazo mara baada ya aya ya 11:

“12. uteketezaji wa vifaa na bidhaa zilizoisha muda wake, ada ya shilingi laki tatu (300,000/=);

13. kumwaga maji taka, ada shilingi elfu thelathini (30,000/=)”.

Lakari ya Halmashauri ya Wilaya ya shinyanga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano uliofanyika tarehe 23-25/3/2023 Mwaka 2022 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya;-

MWL. ALEXIUS REVOCATUS KAGUNZE
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Manispaa Shinyanga*

MH. ELIAS RAMADHAN MASUMBUKO
*Mstahiki Meya wa Halmashauri*
*ya Manispaa ya Shinyanga*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*